**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 6, Issue 1, 2023**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Mwathiriano Kati ya Watunzi wa Riwaya ya Kiswahili: Mwangwi wa Maudhui ya Mafuta (2008) katika Cheche za Moto (2008)

*Felix Musyoka Kalingwa[1*] na Dkt. Titus Musyoka Kaui, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Kenyatta, S. L. P. 43844-00100. Nairobi, Kenya
[*] ORCID ID: https://orcid/0000-0002-9763-1428; Barua pepe ya mawasiliano: kalingwamusyoka@students.ku.ac.ke

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1524**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*18 Oktoba 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Athari, Mwingiliano, Matini, Watunzi, Riwaya.*

**IKISIRI**

Makala hii inashughulikia athari za Katama Mkangi kwa John Habwe kwa kujikita katika riwaya teule za Kiswahili za Mafuta (1984) na Cheche za Moto (2008). Utanzu wa riwaya ya Kiswahili umeendelea kupanuka kimaudhui na kifani kutokana na juhudi za watunzi mbalimbali kama vile Katama Mkangi na John Habwe. Japo tafiti za awali zimetafitia suala la mwingiliano matini, tafiti nyingi zimejikita katika kazi za mtunzi mmoja. Utafiti wa kina ulihitajika kuchunguza namna utunzi wa Mafuta (1984) ulivyoathiri John Habwe alipoitunga riwaya yake ya Cheche za Moto (2008). Katama Mkangi aliandika riwaya ya Mafuta katika wakati wa chama kimoja cha kisiasa ambapo uhuru wa kujieleza ulikuwa umebanwa sana. Habwe ameandika kazi yake katika mazingira yaleyale lakini katika kipindi ambapo uhuru wa kujieleza umepanuliwa. Kwa hivyo, amekwepa mtindo wa kimajazi alioutumia Mkangi na kuyaangazia masuala anayoyaibua kwa njia wazi. Makala hii ililenga kuonyesha kuwa maudhui katika riwaya ya Cheche za Moto ni mwangwi unaotokana na riwaya ya Mafuta (1984). Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya mwingiliano matini iliyoasisiwa na Julia Kristeva (1969). Mihimili mikuu ya nadharia hii iliyoongoza utafiti huu ni pamoja na: hakuna matini ya fasihi yenye sifa za pekee, matini hubainisha sifa mbalimbali za matini tangulizi, na mwisho, matini ya baadaye huweza kufafanua dhana fulani kutoka matini tangulizi kwa njia inayoeleweka. Nadharia hii ya mwingiliano matini ilisaidia pakubwa kuonyesha namna kazi ya awali, Mafuta (1984) ilivyomwathiri John Habwe katika utunzi wa Cheche za Moto (2008) kimaudhui. Riwaya teule ziliteuliwa kimakusudi ili kupata sampuli faafu yenye data ya kujaza pengo la utafiti. Data ilikusanywa kupitia kwa usomaji wa maktabani na vilevile kusakura mitandaoni kuhusu vipengele vya mwingiliano matini katika riwaya ya Kiswahili. Data hii imewasilishwa kwa njia ya kimaelezo. Utafiti wa makala hii unatarajiwa kutoa mchango katika uhakiki wa utanzu wa riwaya ya Kiswahili, hususan kuhusu kipengele cha kuathiriana baina ya watunzi wa riwaya za Kiswahili.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

**APA CITATION**

Kalingwa, F. M. & Kaui, T. M. (2023). Mwathiriano Kati ya Watunzi wa Riwaya ya Kiswahili: Mwangwi wa Maudhui ya Mafuta (2008) katika Cheche za Moto (2008). *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(1), 394-402. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1524.

**CHICAGO CITATION**

Kalingwa, Felix Musyoka and Titus Musyoka Kaui. 2023. "Mwathiriano Kati ya Watunzi wa Riwaya ya Kiswahili: Mwangwi wa Maudhui ya Mafuta (2008) katika Cheche za Moto (2008)". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (1), 394-402. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1524.

**HARVARD CITATION**

Kalingwa, F. M. & Kaui, T. M. (2023) "Mwathiriano Kati ya Watunzi wa Riwaya ya Kiswahili: Mwangwi wa Maudhui ya Mafuta (2008) katika Cheche za Moto (2008)", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), pp. 394-402. doi: 10.37284/jammk.6.1.1524.

**IEEE CITATION**

F. M. Kalingwa & T. M. Kaui "Mwathiriano Kati ya Watunzi wa Riwaya ya Kiswahili: Mwangwi wa Maudhui ya Mafuta (2008) katika Cheche za Moto (2008)", *EAJSS*, vol. 6, no. 1, pp. 394-402, Oct. 2023.

**MLA CITATION**

Kalingwa, Felix Musyoka & Titus Musyoka Kaui. "Mwathiriano Kati ya Watunzi wa Riwaya ya Kiswahili: Mwangwi wa Maudhui ya Mafuta (2008) katika Cheche za Moto (2008)". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 1, Oct. 2023, pp. 394-402, doi:10.37284/jammk.6.1.1524.

## UTANGULIZI

Athari ni dhana iliyofasiriwa na wataalam mbalimbali. Wafula (2015) anaeleza athari kama hali inayomfanya mtunzi kuumba maana ya matini kwa kuihusisha na nyingine. Clayton na Rothstein (1991) wanaeleza athari kama hali ambapo kazi ya mtunzi mmoja hujitokeza moja kwa moja katika kazi nyingine, hata kama waandishi wake ni tofauti kiuzoefu, kiwakati, kimazingira na kijamii.

Katama Mkangi na John Habwe wamechangia pakubwa katika ukuaji wa utanzu wa riwaya. Wamezitunga riwaya anuwai. Katama Mkangi aliziandika riwaya za *Ukiwa* (1975), *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995). Kwa upande wake, John Habwe ameziandika riwaya zifuatazo: *Maumbile si Huja* (1995), *Maisha Kitendawili* (2000), *Paradiso* (2005), *Safari ya Lamu* (2006), *Kovu Moyoni* (2014) na *Hidaya yangu* (2018). Makala hii inaangazia athari za Katama Mkangi kwa John Habwe katika kiwango cha maudhui.

## NADHARIA

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya mwingiliano matini. Nadharia hii iliasisiwa na Mfaransa Julia Kristeva mnamo mwaka wa 1969. Mishra (2012) anabainisha kuwa dhana ya mwingiliano matini ilitumiwa kwa mara ya kwanza na Julia Kristeva mnamo mwaka wa 1966 katika kazi zake za *The bounded text* na *Word*. Katika kazi za awali kuhusu nadharia hii yake, Kristeva anahoji kuwa watunzi hawatungi matini kutokana na mawazo yao, ila uandishi wao hutokana na kuathiriwa na matini za awali. Clayton na Rothstein (1991) katika *Influence and Intertextuality in Literary History*, alihoji kuwa kauli kadha kutoka matini nyingine zinahusiana na kuathiriana. Mtazamo huu ulitufaa katika kuonyesha namna maudhui katika *Cheche za Moto* (2008) ni mwangwi unaotokana na *Mafuta* (1984).

Akimnukuu Kristeva (1980), Nabangi (2013) anaeleza kuwa mwingiliano matini ni uzalishaji wa maana ndani ya matini wala sio ndani ya mahusiano kati ya matini mbalimbali. Kwa mujibu wa maelezo haya, nadharia hii imeufaa utafiti huu katika kuonyesha namna dhana mbalimbali zilizowasilishwa kimajazi kutokana na udikteta wakati wa miaka ya themanini, katika riwaya ya *Mafuta* (1984) zinavyofafanuliwa kwa uwazi katika riwaya ya *Cheche za Moto* (2008). Riwaya ya *Cheche za Moto* iliandikwa wakati uhuru wa kujieleza ulikuwa umepanuka. Mtunzi aliyaeleza maovu kwa njia ya wazi. Wamitila (2002) anaeleza kuwa kazi ya fasihi haiwezi kujitegemea kwani

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1524

kueleweka kwake hutegemea kuwepo kwa matini ya awali inayohusiana nayo. Mwandishi anapoanza kuandika matini yake, huwa katika hali ya kumjibu, kumwuliza au kumchangia mtangulizi wake.

## MBINU ZA KUKUSANYA DATA

Utafiti huu umefanyiwa maktabani. Ili kukusanya data mwafaka ya kuziba pengo la utafiti, riwaya teule za *Mafuta* (1984) na *Cheche za Moto* (2008) zilisomwa kwa kina na kuchanganuliwa. Data inayohusiana na mada ya utafiti ilidondolewa kutoka kwenye riwaya teule. Ili kupata data kuhusu yaliyochapishwa na msingi wa nadharia, vitabu, majarida na tasnifu mbalimbali zilisomwa. Isitoshe, utafiti huu uliweza kusakura mitandaoni ili kupata tafiti za hivi punde zaidi kutoka maeneo mbalimbali. Mbinu ya usampulishaji iliyotumiwa na utafiti huu ni ya kimakusudi. Riwaya teule za *Mafuta* (1984) na *Cheche za Moto* (2008) zimechaguliwa kwani ziliupa utafiti huu data inayoafikiana na malengo ya utafiti. Utafiti huu umechanganua data hii kwa njia ya kimaelezo.

## MATOKEO

### Mfumo wa Utawala wa Kidikteta

Maitaria (2014) anafafanua utawala wa kidikteta kama unaowafanya viongozi kupuuza maoni ya watawaliwa. Chacha (1992) alihoji kuwa vyama huwa na uwezo wa kutetea haki za watu zinapokiukwa. Watunzi wa riwaya teule katika utafiti huu wamebaini kuwa watawaliwa wamepuuzwa katika mchakato wa uongozi. Katama Mkangi anabainisha hili anaposema:

> *Hakuna ruhusa ya kuuliza swali, kujibu chochote au kutoa wazo lolote…* (Riwaya ya *Mafuta*, Ukurasa 49)

Katama Mkangi anabainisha namna wanajamii wanapokoseshwa uwezo wa kushirikishwa katika maamuzi ya mustakabali wao. Matope anaamuliwa kunyongwa hata bila kushirikishwa. John Habwe anabainisha hali hii ya kukandamiza maoni ya watawaliwa anapotoa kauli ifuatayo:

> *Kwa nini mna chama cha upinzani hali sheria inapinga vyama vya aina hiyo?* (*Cheche za Moto*, ukurasa 90)

Kauli hii ina maana kuwa wananchi hawana kibali cha kutoa maoni yao kwa kunyimwa uwezo wa kuwa na vyama vya upinzani.

Wafula & Mue (2021) alifafanua dhuluma kama sifa mojawapo ya utawala wa kidikteta. Aliendelea kusema kuwa dhuluma hizi huhitaji kupingwa katika jamii. Jamii yenye dhuluma huwa imetawaliwa na woga hususan wanyonge wanapoogopa mateso kutoka kwa makundi mbalimbali. Watunzi wa riwaya teule wamebainisha asasi dhulumati kwa njia ya kimwingiliano matini.

Mkangi anawatumia vibaraka wenye mamlaka makubwa kuwaonea yakhe. Mkangi anatumia dayolojia baina ya Ti na Mtue kuonesha maonevu kwa wanyonge. Anasema:

> *Kule ulikomwona akienda ni kwake ofisini. Yeye kama tuseme, Waziri wa Mguu wa Kulia ya Mbele, anao wasaidizi chungu nzima ingawaje madaraka yote ni yake* (Riwaya ya *Mafuta*, ukurasa 18)

Katama Mkangi anaficha nyuso za watesi hawa kwa kuepuka kubainisha majina yao halisi na vyeo vyeo halisi. Hali hii inatokana na udikteta uliokuwepo katika mazingira ya mtunzi alipoiandika kazi yake miaka ya themanini. Anabainisha uwezo wa vibaraka hawa anaposema:

> *Vimemfanya kuwa mtu wa hasira za haraka zisizohitaji kuchokozwa…Na kwa mtu yeyote kuonyesha ufedhuli aghalabu hunyongwa…; shukuru sana malaika wako…* (Riwaya ya *Mafuta*, ukurasa 18)

John Habwe anabainisha kuwa watuhumiwa hawakupewa nafasi ya kujitetea. Anatumia sauti ya

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1524

watesi wa Mule katika Dhiki House kubainisha dhuluma kwa wanyonge. Anasema:

> *"Profesa ukiwa karibu kusema utatwambia ili usiumie sana"* (Riwaya ya *Cheche za Moto*, ukurasa 41)

Tofauti na Katama Mkangi, John Habwe anafichua nyuso za watesi hawa na kuwabainisha kandamnasi. John Habwe anasema:

> *Kisa kimoja ambacho Mule alitambiwa na ambacho hatosahau kilihusu Mohamed Yahaya. Mohamed alikuwa na mke aliyeitwa Fauziya. Alipokuwa yeye na mkewe katika sherehe, huyo mkewe alihitajika na Osman Jumbe. Mohamed alipaswa kumpeleka mwenyewe. Mtu alikwenda na mkewe. Mkewe akamaliza shughuli yake na Osman Jumbe kisha Mohamed akapewa jozi ya viatu. Baadaye wote wawili, mtu na mkewe walipigwa risasi usiku* (Riwaya ya *Cheche za Moto*, ukurasa 116)

John Habwe anataja kiongozi wa nchi, Osman Jumbe kama anayeendeleza dhuluma. Kumbainisha huku kunaashiria kuwa uwezo wa kujieleza ulikuwa umepanuka wakati wa utunzi wa riwaya ya *Cheche za Moto* (2008) tofauti na ilivyokuwa wakati wa utunzi wa *Mafuta* (1984).

Omoga (2018) anaeleza kuwa watawaliwa huwa wategemezi wasio na nguvu. Hali hii huwafanya kushawishiwa kwa visababu kadha wa kadha. Kwa kuogopa mateso na dhuluma za walio na nguvu, watawaliwa huogopa kushiriki kikamilifu katika uongozi. Hata hivyo, Oketch na wenzie (2020) wanasema kuwa vijana wana jukumu ya kuikomboa jamii kutoka kwa dhuluma za madikteta. Kaui (2008) amewaeleza vijana kama wanadamu wenye fahamu zao na ambao kisheria na kijamii wamefikia umri wa kuoa au kuolewa ingawa wanaishi chini ya uangalizi wa wazazi wao.

Watunzi wa *Mafuta* na *Cheche za Moto* wameingiliana katika kukuza nafasi ya vijana katika kuukabili mfumo wa udikteta. Katama Mkangi anabainisha nafasi ya vijana kupitia uhusika wa Ti. Ti aliwazindua wanyonge kwa kuwaelezea kadhia yake. Ti anasema:

> *Cha muhimu ni sisi soteni kukubali kwamba, wengi wa hawa walijitolea mhanga ili kusisitiza kuwa uhuru wa mtu ni ukweli usiopingika (Riwaya ya Mafuta, ukurasa 77)*

Wakiwa kwa Msati, Ti anawafafanulia wanyonge namna wanavyotumia uwongo kujidumisha mamlakani. Hali hii inawafungua macho na kuwashajiisha hadi wakaenda kuwafungulia Mtue na Matope walipofungiwa. Hatima ya zoezi hili lilikuwa kuangushwa kwa utawala wa kidikteta wa Wateule.

Mwongela (2021) anakubaliana na mawazo ya Fakih (2017) anayetambua kuwa mwanamke ni mhusika binadamu kama wanadamu wengine na aliyetunukiwa uwezo mkubwa wa kutenda mambo mbalimbali. Wanawake katika riwaya teule wamechukua nafasi chanya katika utetezi wa masilahi ya umma. Kwa mfano, kama Katama Mkangi alivyomtumia mwanamke kijana Ti kuikomboa jamii yake, John Habwe anamtumia Fatuma kwa njia inayobainisha athari ya watunzi. Anasema:

> *Labda Fatuma hakutaka kuamini ati mwafrika amelaaniwa… Cheche ilikuwa kama uraibu…Fatuma hakutaka kurudi nyuma alitaka kwenda mbele. Alijua huko mbele kuna hatari lakini alijua mapambano yasipokuwa na kafara hayakamiliki* (Riwaya ya *Cheche za Moto*, ukurusa 266)

Fatuma aliendeleza juhudi za ukombozi wa jamii baada ya kutoweka kwa mumewe Profesa Mule. Hatimaye juhudi zake zilimwondoa dikteta Rais Mtanda uongozini.

**Mfumo wa Kijamii**

Oketch na wenzie (2020) wanashadidia kuwa jukumu la fasihi ni kueleza jamii namna ilivyo. Wanaendelea kukubaliana kuwa ili fasihi ifafanue jamii husika vilivyo, sharti itumie lugha ya wanajamii husika kufafanua imani na dini,

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

utamaduni, nafasi ya elimu, masuala ya jinsia na uana, hali ya maisha na maadili katika jamii. Watunzi wa riwaya teule wamefanikiwa kuifafanua jamii kwa kubainisha vipengele hivi kwenye kazi zao tofauti.

***Imani na Dini***

Kilonzo (2012) anaeleza dini kuwa mkusanyiko wa imani, desturi na asasi ambazo binadamu katika jamii zote zinazojulikana wamezizua kama majibu kwa zile sehemu za maisha wanazohisi haziwezi kueleweka. Katama Mkangi alionyesha nafasi ya dini katika kutekeleza maovu katika riwaya ya *Mafuta* (1984). Alionyesha kuwa maovu mengi kwa walalahoi yanaidhinishwa kwa misingi ya dini. Tabaka la juu lilihalalisha maslahi yao kwa kuzua jina la Mungu. Mkangi anabainisha haya anaposeama:

> *Alijisifu na kusema kazi hii mahsusi na, ya maana, ni Mungu mwenyewe ndiye aliyemtunukia…alilipwa maridhawa…* (Riwaya ya *Mafuta*, ukurasa 67)

Kifungu hiki kinatuchorea jamii ambayo walio na nafasi wanawatesa wengine. Inawabidi hata kutafuta visingizio vya kuendeleza maovu hayo mojawapo ikiwa ni dini.

Kwa kuathirka na Mkangi, John Habwe vilevile katika riwaya ya *Cheche za Moto*, amedhihirisha kuwa dini imetumika kuhalalisha ufisadi na ubadhirifu wa mali ya umma. John Habwe anadokeza hayo anapoandika:

> *Adhiambo aliamini siku ya mtu ni moja ambayo Rabana humfungulia vilango vya kupitia akawa pia yeye ni mtu wa kuselelea katika magari makubwa makubwa yaliyoendeshwa kwa mali ya umma* (Riwaya ya *Cheche za Moto*, ukurasa wa 157)

**Utabaka**

Kamusi ya Kiswahili sanifu (2015) inafafanua utabaka kama mgawanyo baina ya wanajamii kwa msingi wa mali. Wanajamii hugawika katika makundi mawili: walio na mali na wanyonge. Watunzi wa riwaya teule wameonyesha kuwa utabaka una madhara mengi katika jamii. Watunzi wamehusiana katika kuwasilisha madhara haya ya utabaka.

***Utabaka na Viwango Vyake Mbalimbali***

Katama Mkangi na John Habwe wamebainisha kuwa kuna tofauti za wazi baina ya tabaka moja na nyingine. Aidha, kati ya watu wa tabaka moja, kunatokea kuwa wengine ni afadhali kuliko wenzao. Tazama mawazo ya Dubwana akimrejelea Ti:

> *Pia usisahau uliapa ya kwamba, wewe kama mteule, hungecheka mteule mwingine- sembuse sisi mijiteule ya wateule?* (Riwaya ya *Mafuta*, ukurasa 49)

Kifungu hiki kinabainisha kuwa hata katika tabaka moja la juu, mna tofauti baina yao na kwamba hakuna usawa. Mtue anaishia kuitwa Mteule marufuku kwani alituhumiwa kuwa wa tabaka la chini. Tofauti hizi za kitabaka katika tabaka moja ndizo zinazochangia Mtue kufungwa huku mteule mwenzake aliyecheka, Ti, akiachiliwa huru.

John Habwe anaonyesha mwingiliano na anayoyazua Katama Mkangi. Anaeleza kuwa watu katika tabaka moja hawana madaraka yanayotoshana. Kuna wale ambao wana majukumu mengi kuliko wengine. Kati ya wafanyakazi wengi alio nao kiongozi, kuna wale anaoaminia na wengine. Anaowaamini wana nafasi kubwa katika utawala. Nandi anawaza akilini namna nafasi yake ilivyochukuliwa na Omari. Anasema maneno yafuatayo:

> *Yeye Omari alikuwa waziri wa Misitu na alikuwa katika watu walioaminiwa na Mtanda baada yake yeye kudondoshwa* (Riwaya ya *Cheche za Moto*, ukurasa 161)

***Utabaka na Uwongo***

Riwaya teule zimebainisha kuwa tabaka la juu aghalabu hutumia uwongo kujidumisha mamlakani.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Mathalani, riwaya ya *Mafuta* inaeleza hali hii. Uzungumzi nafsia wa Matope unadokeza kuwa tabaka la juu daima husema uwongo ili kuendeleza utawala wao. Katama Mkangi anasema haya anapoandika yafuatayo:

> *Mmefanya uongo ukawa ukweli na ukweli, uongo…Mmepindua hata sheria za Maumbile ili kumamatia enzi yenu…* (Riwaya ya *Mafuta*, ukurasa 40)

Isitoshe, inabainika kuwa wanaojaribu kuwagutusha maskini kwa kuwaambia ukweli waliteswa sana. Viongozi wa tabaka la juu waliupinga ukweli ili kuendelea kujidumisha mamlakani. Mkangi anaeleza haya anaposema:

> *Na kama ujuavyo, msema kweli yeyote ni adui yetu na ni lazima anyamazishwe kwa kum 'krii.'*(Riwaya ya *Mafuta*, ukurasa 87)

John Habwe anayafafanua aliyoyawasilisha mkangi kwa namna rahisi. Anaeleza kuwa ili kujidumisha uongozini, inawabidi viongozi katili kutumia uwongo na propaganda.

> *Tumeamua kukuachilia lakini uhakikishe husomi tena hicho kitabu. Ni kitabu kinachopotosha watu akili kwa hivyo ukitupe mbali* (Riwaya ya *Cheche za Moto*, Ukurasa 37)

Masaba anajipata kwa shida baada ya kusoma kitabu cha *Cheche za Moto*. Askari wanamweleza kuwa ni kitabu kinachowapotosha watu akili. Ukweli ni kwamba, baada ya kusoma kitabu hicho, wasomi walifahamu namna serikali zinavyowapuuza wanyonge. Serikali inatumia mbinu ya uwongo kuhakikisha wananchi hawakisomi na kupata ukweli.

***Utabaka na Usaliti***

Juhudi za kujidumisha kwenye tabaka la juu huendeleza usaliti katika jamii. Wanajamii ambao hawana haki ya kujiendeleza huweza kusalitiwa. Katama Mkangi anadhihirisha usaliti unaotokana na utabaka anaposema:

> *Maskini mwanamke wa watu…Mafuta yake yote yashaoshwa* (Riwaya ya *Mafuta*, ukurasa 19)

Mama Fofi aliyatimiza masharti makali ya kuwa mteule. Japo hivyo, hakuweza kukilalia kitanda kwani *Mafuta* yalioshwa kwa maji. Hali hii ina maana kuwa hata maskini wanapotia bidii namna gani, huweza kusalitiwa kwa kukoseshwa nafasi ya kuwa viongozi katika jamii kandamizi.

Utunzi wa John Habwe vilevile unabainisha kuwa usaliti ni zao la utabaka. Watu kwa kupenda mali, wanapuuzilia mbali maslahi ya walio wengi. Tazama mawazo ya Mule kwenye *Cheche za Moto*.

> *Alifikiria uhuru katika bara la Afrika. Waliopigania uhuru sio waliopata matunda* (Riwaya ya *Cheche za Moto*, ukurasa 105)

Kifungu hiki kinatuchorea namna bidii ya tabaka la chini inavyowasaidia kupata matunda. Baada ya ushindi huu, maskini hawa walipuuzwa na walio na vyeo. Huu ni usaliti wa juhudi zao.

**Mfumo wa Kiuchumi wa Kibepari**

Kwa mujibu wa Njogu (1997) kuna njia mbalimbali za uzalishaji mali katika jamii. Njia hizi ni pamoja na: ujima, utumwa, umwinyi, ubepari, ujamaa na ukomunisti. Riwaya teule za utafiti huu zimedhihirisha ubepari kama njia tawala ya nyenzo ya uzalishaji mali. Katama Mkangi alieleza ubepari kwa njia ya kimafumbo inayomfanya John Habwe aufafanue kikamilifu baada ya uhuru wa kujielezaa uliporuhusiwa.

Njogu (1997) anaeleza ubepari kama mfumo wa uzalishaji mali ambapo umiliki wa mali huwa wa kibinafsi kwa nia ya kujinufaisha zaidi. Mabwanyenye huwatunza wanyonge kufanya kazi nyingi kwa mishahara midogo. Watunzi wa *Mafuta* na *Cheche za Moto* wanadhihirisha ubepari katika kazi zao.

Maskini wa tabaka la chini wanafanyizwa kazi ngumu yenye mshahara haba. Haya yote ni kwa ajili

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1524

ya kumpa uwezo bwanyenye kuzidi kuongeza uwezo wake wa kuwadhulumu wasionacho. Mkangi anabainisha hili anaposema haya kupitia usimulizi wa Mama Fofi mle mduarani:

> *Kulikuwa na wale ambao walipewa kandarasi ya kukamata kumbikumbi baada ya kudodosha bawa zao. Hawa, chao kilikuwa kidari. Nyama za mbavu zikawa zetu* (Riwaya ya *Mafuta*, ukurasa 30-31)

Kifungu hiki kinadhihirisha kuwa wananchi wa tabaka la chini hawana uwezo wa kuzalisha mali. Mtunzi anawaita wa 'kulalia tundu tu'. Inawabidi matajiri wenye uwezo kuwaajiri kazi wanayowalipa 'kidari' na kubakia na 'nyama ya mbavu'. Maana ya kifungu hiki ni kuwa tabaka la mabepari linawatumikisha wanyonge kwa faida yao.

John Habwe anadhihirisha utumwa kwa wanyonge anapofafanua namna wakoloni wanavyowatumikisha wanyonge. John Habwe anasema haya katika kazi yake:

> *Lazima tutafute mbinu za kuwahadaa. Mafuska wakubwa sana wao. Angalia, eeeh? Wametutawala.Aaa! Mwanzo walitufanya watumwa tukatajirisha dola zao kule Marekani na Ulaya* (Riwaya ya *Cheche za Moto*, ukurasa 129)

Kukosa nyenzo za uzalishaji mali husababisha uzururaji. Kwa mujibu wa Al- Amin Mazrui (1979), wazururaji ni watu hatari sana ambao daima huwa tayari kufanya lolote. Hata bila malipo yoyote, wazururaji hawa wako radhi kutumika na wenye nacho kuzua rabsha. Mkangi anadokeza haya anapowarejelea wazururaji waliotishia kumwangamiza Jali. Anasema:

> *Huku wakipiga mayowe ya 'mwizi huyoo…mwizi huyoo…mwizi huyoo…Umati wa wasio na la kufanya (kwa kukosa njia za uzalishaji mali) ulimwandama na hukumu ya kifo ikiwa mwao machoni* (Riwaya ya *Mafuta*, ukurasa 5)

Kisa hiki cha kuwepo na watu wengi wasio na la kufanya, kinahatarisha maisha ya Jali, kwani bila hata kuahidiwa malipo yoyote, wako radhi kumwua mmoja wao bila hata kuuliza swali. Mwenye mkunazi anaifurahia hali hii japo wazururaji hawa walimwibia. Anaamini kisa hiki kitawaogofya wanyonge na kumwacha aendeleze ubepari.

John Habwe anafuata mkondo wa Mkangi anapoeleza kuwepo kwa wachache wanaotumiwa na viongozi kuendeleza maovu ili kupata malipo. Anawasilisha haya kwa kutumia askari wanaotumiwa na utawala kuwanyanyasa wanyonge. Anasema:

> *Inspekta Banda anakubali kazi yake ni mzigo mkubwa kwake. Shukrani yake ni shamba kubwa pwani. Mtu mwingine aliye na shamba la kiasi chake ni Babu ambaye shamba lake la mikanju limepakana na lake la miembe* (Riwaya ya *Cheche za Moto*, ukurasa 87)

Inspekta Babu na Banda wanatumiwa kuwatesa wanaoyaangazia maovu ya viongozi. Kutokana na kazi hii yao ya kudhulumu wanyonge, wanalipwa kwa mashamba makubwa.

Kimwea (2019) akifafanua mfumo wa ubepari, anaueleza kama mfumo ambao walio wengi hawana chochote ila nguvu zao ambazo huweza kuziuza kupata mishahara midogo ya kujikimu. Katama Mkangi anaonyesha hali hii ya maskini kudunishwa kwakulipwa kwa mafungu ya kunazi.

> *Si tu kila siku alipoamka, aliwapatia fungu moja: wangemwendea kinyume namna gani?* (Riwaya ya *Mafuta*, ukurasa 1)

Zuka na Kazamoyo wanalipwa kwa mafungu ya kunazi ili kuyalinda mengine mwenye mkunazi anapolala. Huku ni kutumia nguvu zao kwa faida yake mwenyewe.

John Habwe anafafanua hali hii ya kupokwa nguvu kwa yakhe. Wafungwa wanapolazimishwa kufanya kazi kwa wakubwa serikalini. Mahabusu hawa wanatumiwa na seikali kujinufaisha bila kupata chochote. Mtunzi wa *Cheche za Moto* anaeleza haya anaposema:

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1524

> *Kama wamefungua huwa wamekwenda kufanya kazi katika shamba la mojawapo katika mawaziri, au katibu wa kudumu au hata mkurungezi fulani…* (Riwaya ya *Cheche za Moto*, ukurasa 131)

## HITIMISHO

Makala hii imeangazia jinsi Katama Mkangi alivyomwathiri John Habwe kimaudhui. Maudhui mbalimbali yanayoubainisha mwathiriano huu yamefafanuliwa kikamilifu. Haya ni kama vile mfumo wa kiutawala wa kidikteta, ubepari na ule wa kijamii. Watunzi wa riwaya teule wamebainisha mielekeo sawa katika kukuza maudhui hayo.

Imebainika kuwa John Habwe ameathirika na Mkangi na anayafafanua maudhui anayoyazua Mkangi ya kimafumbo katika *Mafuta*. Riwaya yake ya hivi punde ya *Cheche za Moto* inaangazia yaliyomo katika *Mafuta* lakini kwa njia ya uwazi kutokana na ukuaji wa demokrasia na kupanuka kwa uhuru wa kujieleza.

## MAREJELEO


BAKITA (2015). *Kamusi kuu ya Kiswahili*. Dar es Salaam.Longhorn Publishers.

Clayton, J. & Rotherstein, E. (1991). *Figures in the Corpus:Theories of Influence and Intertexuality*. Madison, Wisconsin:University of Winconsin Press Uk 3-35

Chacha, N. C. (1980) Ushairi wa Abdilatif Abdalla. Nairobi. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)

Fakih, S. J. (2017). Kutathmini Mabadiliko ya Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya ya Utengano na Kamwe si Mbali Tena. Tasnifu ya M.A (isiyochapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

Habwe, J. (2008). *Cheche za Moto*. Nairobi.Jomo Kenyatta Foundation.

Kaui T. M (2008). Usawiri wa Vijana katika Tamthilia Teule za Kiswahili. Chuo Kikuu cha Kenyatta

Kilonzo (2012) . Ujitambuzi na Utambulisho wa Kijinsia katika Riwaya ya Maisha Kitendawili. Chuo Kikuu cha Nairobi

Kimwea (2019). Taswira ya Jamii katika Riwaya ya Yasinya na Mwanaisha. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kristeva, J. (1969). *Desire in Language: Asemiotic Approach to Literature and Art*.New York.Colombia University Press.

Maitaria, J. N (2014). Dhima ya Ushairi wa Kiswahili katika Kuelimisha Jamii kuhusu Demokrasia. Kiswahili Juzuu 77.

Mishra, R.K (2012). '*A Study of Intertextuality: The Way of Reading and Writing*.' Katika Prime Journals. http://primejournal.org/PRE/pdf/11/10/2023

Mkangi, K. (1984). *Mafuta*. Nairobi.Heinamann Educational Books

Mwongela (2021) . Usimulizi katika Riwaya ya Trilojia ya Kiswahili: Mfano wa Siri Sirini.

Nabangi, J.K (2013). Athari za Utenzi katika Uandishi wa Riwaya Teule ya Kiswahili: Tasnifu ya uzamili(isiyochapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Njogu, K(1997). Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar. Nairobi: Nairobi University Press.

Oketch, S., Ambuyo, B., & Makokha, R. (2020). Mifumo ya Kijamii katika Tamthilia Teule za Kiswahili. East African Journal of Swahili Studies, 2(1), 8-18. https://doi.org/10.37284/eajss.2.1.135.

Omoga, R. G (2018). Mwananchi kama mdhulumu wa Maslahi yake katika Tamthilia za Kilio cha

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1524

Haki, Amezidi na Mstahiki Meya. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Shemwata (2021). Itikadi katika Tamthilia ya Emmanuel Mbogo: Utafiti (isiyochapishwa) Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Wafula & Mue (2021). Uchanganuzi wa Riwaya ya Kiza katika Nuru ya Said Ahmed Mohammed kwa Misingi ya Umarxi mpya wa Kifreire. Swahili Forum 28: 34-45

Wafula P.K (2015). Mwingilianomatini katika Cheche za Moto na Kidagaa Kimemwozea. Chuo Kikuu cha Kenyatta

Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi.Focus Publishers

Wamitila, K. (2006). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi ya vipengele vyake*.Nairobi.Phoenix Publishers Limited

Wamitila, K. (2008). *Misingi ya Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi.Vide-Muwa Publishers

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.